*Kioo cha Lugha, Juz. 21(2), 298-311*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i2.8

# Matumizi ya Nahau katika Ujarabati wa Mikakati ya Kisintaksia ya Usimbaji wa Fokasi katika Sentensi za Kiswahili

*Elishafati J. Ndumiwe*[1] *na Amani Lusekelo*[2]

## Ikisiri

Usimbaji wa fokasi katika sentensi za lugha za Kibantu hufanyika kwa kutumia mikakati mbalimbali ya kimofolojia, kisintaksia au kifonolojia (van der Wal, 2009; Yonenda, 2011; Morimoto, 2014; Ndumiwe, 2023). Aidha, kuna mbinu tofautitofauti zinazotumika kung'amua ikiwa mikakati madhukura inasimba fokasi au la. Mojawapo ya mbinu hizo ni matumizi ya nahau. Van der Wal (2016, 2021) alichunguza mbinu hiyo katika ung'amuzi wa usimbaji wa fokasi katika lugha za Kimakua (P31), Kizulu (S42), Kimatengo (N13), Kirundi (JD62), Kichangana (S53), Kiganda (JE15), Kinyakyusa (M31), Kibukusu (JD31c) na Kitharaka (E54). Hata hivyo, hakuna utafiti uliofanyika katika lugha ya Kiswahili (G42) kuhusu matumizi ya nahau katika ujarabati wa mikakati ya usimbaji wa fokasi. Kwa hiyo, lengo la makala hii ni kuhakiki mikakati ya kisintakisa ya usimbaji wa fokasi kwa kutumia nahau za Kiswahili. Data zimekusanywa kwa kutumia mbinu za usaili na upitiaji wa nyaraka. Data hizo zimechambuliwa kitaamuli kwa kuongozwa na Nadharia ya Vibadala vya Kisemantiki (Rooth, 2016). Utafiti huu umebainisha kuwa nahau za Kiswahili zikiundiwa sentensi kwa kutumia mikakati ya ukasimishaji, upinduzi wa viambajengo na utenguaji kushoto, maana ya nahau inatoweka. Kwa hiyo, utowekaji wa maana ya nahau huthibitisha kuwa mikakati husika hutumika kusimba fokasi katika lugha ya Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Fokasi ni kiambajengo cha sentensi kinachobeba taarifa mpya katika sentensi husika na chenye uwezo wa kuchochea seti ya vibadala katika nafasi kinapotokea (Krifka, 2007). Katika lugha ya Kiswahili, kiambajengo hicho hutokea kiasilia mara baada ya kitenzi ikiwa sentensi ina kitenzi elekezi (Mungania na Schroeder, 2018). Aidha, sentensi ikijengwa na kitenzi sielekezi, kirai kitenzi ndicho hubeba fokasi katika sentensi husika (Ndumiwe, 2022b). Vilevile, fokasi huweza kutokea katika mazingira yasiyo asilia, yaani kabla ya kitenzi, kutokana na upanguaji wa

[1] Mhadhiri, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Mt. Agustino, Tanzania. Baruapepe: ndumiweelisha@gmail.com
[2] Profesa Mshiriki, Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: amanilusekelo@gmail.com

mpangilio wa kawaida wa maneno katika sentensi husika (Yonenda, 2011; Mwamzandi, 2014).

Katika lugha ya Kiswahili, fokasi hudhihirishwa kwa kutumia sifa kadhaa. Kwanza, fokasi ni kiambajengo chenye vibadala vya kimuktadha. Nafasi inayokaliwa na fokasi katika sentensi huweza kukaliwa na kibadala kingine. Mathalani, ikiwa nomino inayobeba fokasi hutokea katika ngeli ya kwanza, kibadala chake hutokea katika ngeli ya kwanza pia. Pili, fokasi huulizwa kwa kutumia maneno ulizi katika nafasi yake. Mara nyingi, maneno ulizi yanayotumika katika nafasi ya fokasi ni wapi, nini au nani. Mifano ya 1(a) na (b) inathibitisha haya:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. (a) | ki-tabu | ki-li-fich-w-a | **wapi**? |
| | kng7-tabu | kp7-knj-fich-tndw-kt[3] | wapi |
| | ‘kitabu kilifichwa wapi?’ | | |
| | **Chanzo**: Hassan (2019) | | |
| (b) | **nini** | w-anafunzi | wa-me-ki-tekelez-a? |
| | nini | kng2-anafunzi | kp2-tmlf-ky-tekelez-kt |
| | ‘nini wanafunzi wamelitelekeza?’ | | |
| | **Chanzo**: Mkude (2005) | | |

Katika Mfano Na.1(a), jibu linalotokea katika nafasi ya neno ulizi (wapi) ni fokasi. Katika sentensi hiyo, jibu ni mahali ambapo pamefichwa kitabu, kwa mfano, kabatini au uvunguni. Vilevile, katika Mfano Na. 1(b), jibu linalotokea katika nafasi ya neno ulizi (nini) ni fokasi. Katika sentensi hiyo, jibu ni kilichotekelezwa na wanafunzi, kwa mfano, agizo la mwalimu.

Tatu, fokasi huwakilishwa na kiambishi yambwa katika kitenzi cha Kiswahili. Kiambishi hiki hutokea baada ya kiambishi cha njeo au kiambishi cha hali katika kitenzi elekezi kisicho na urejeshi. Katika kitenzi chenye urejeshi, kiambishi yambwa hutokea baada ya kiambishi cha urejeshi kwa ajili ya kupatanisha kitenzi husika na yambwa inayopaswa kujaliza kitenzi husika. Mfano Na. 2 unatoa mwanga kuhusu hilo:

2. (a) mu-alimu a-me-***wa***-nyim-a [**wa-anafunzi]**$_{F}$ ruhusa.

[3] Vifupisho vilivyotumika katika makala hii:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| kng | = | kiambishi ngeli | tmlf | = | hali timilifu |
| kp | = | kiambishi kipatanishi | ku | = | kiambishi cha ukanushi |
| kt | = | kiambishi tamati | krj | = | kiambishi cha urejeshi |
| ktm | = | kiambishi tamati mahali | tndw | = | utendwa |
| ky | = | kiambishi cha yambwa | YKT | = | yambwa-kiima-kitenzi |
| knj | = | kiambishi cha njeo | KN | = | kirai nomino |
| knf | = | kiambishi cha nafsi | KTY | = | kiima-kitenzi-yambwa |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | kng1-alimu | kp1-tmlf-ky-nyim-kt | kng2-anafunzi | ruhusa | | |
| | 'mwalimu amewanyima wanafunzi ruhusa'. | | | | | |
| (b) | **[elimu ya** | **nyota,**$]_F$ wa-tu | ha-wa-***i***-thamini | siku | hizi. | |
| | elimu ya | nyota, kng2-tu | ku-kp2-ky-thamini | siku | hizi | |
| | 'elimu ya nyota watu hawaithamini siku hizi'. | | | | | |

**Chanzo**: Mkude (2005)

Katika Mfano Na. 2(a), kiambishi {-wa-} kilichopachikwa katika kitenzi kinaiwakilisha fokasi (wanafunzi) katika kitenzi. Pia, katika Mfano Na. 2(b), kiambishi {-i-} kilichopachikwa katika kitenzi kinaiwakilisha fokasi (elimu ya nyota). Hata hivyo, kiambishi yambwa hakitokei ikiwa KN-yambwa ni kimahali. Kwa mujibu wa Hassan (2019), kimahali kinapopatanishwa na yambwa huzalisha tungo isiyokubalika. Kwa mfano, sentensi **uchafu ume-pa-tapakaa sokoni* haikubaliki katika Kiswahili kutokana na kuwapo kwa kiambishi cha yambwa katika kitenzi. Kutokana na hilo, Ngonyani (1998) anadokeza kuwa katika mazingira ya baada ya kitenzi katika sentensi za Kiswahili huweza kutokea viambajengo tofautitofauti, kama vile oblikyu, kitumizi, kijalizo au chagizo.

Nne, fokasi hutokea kiasilia mara baada ya kitenzi. Mpangilio wa taarifa katika sentensi za Kiswahili huruhusu taarifa mpya kutokea kiasilia mara baada ya kitenzi (Mwamzandi, 2014; Mungania na Schroeder, 2018). Kimsingi, fokasi hukamilisha taarifa kuhusu kinachoelezwa na kiima. Ndiyo maana hutokea kiasilia mara baada ya kitenzi ili kutoa taarifa kuhusu kiima. Taarifa hiyo huwa ni mpya kwa sababu haipo ndani ya uelewa wa mpokea taarifa. Mathalani, katika Mfano Na. 2(a), fokasi *wanafunzi* imetokea mara baada ya kitenzi. Hata hivyo, upo uwezekano wa fokasi kutokea kabla ya kitenzi ambapo hurejelewa kuwa ni mazingira yasiyo asilia kama inavyoonekana katika 2(b).

Mwisho, fokasi ni kiambajengo cha lazima katika sentensi. Kutokana na sifa hii, uondoaji wa fokasi katika sentensi huacha maswali kwa mpokea taarifa. Hii ni kwa sababu fokasi ni taarifa ambayo msemaji au mwandishi anakusudia imfikie msikilizaji au msomaji. Fokasi inapoondolewa katika sentensi huacha maswali ya wapi, nini, nani au lipi. Kwa mfano, katika sentensi: 'Kitabu cha Kiswahili, anakisoma mtoto'. Fokasi 'kitabu cha Kiswahili' ikiondolewa sentensi itabaki 'anasoma mtoto'. Sentensi iliyobakia haina ujumbe uliokamilika.

Tafiti za awali kuhusu utokeaji wa fokasi katika tungo za Kiswahili zimemakinikia katika mbinu za ung'amuzi wa fokasi na mikakati ya kisarufi inayotumika katika usimbaji wa fokasi katika sentensi (Mwamzandi, 2014; Mungania na Schroeder, 2018; Ndumiwe, 2022a). Kulingana na tafiti hizo, ilibainika kuwa fokasi katika lugha ya Kiswahili husimbwa kwa kutumia mikakati ya kisintaksia tofauti na ilivyo katika lugha ya Kikuyu, Kikuria na Kiganda ambazo hutumia mikakati ya kimofolojia. Aidha, kuna mbinu tofautitofauti zinazotumika kuhakiki ikiwa mikakati madhukura inasimba fokasi au la. Mbinu

zilizopendekezwa zilionekana kutofautiana au kufanana katika lugha kadhaa. Miongoni mwa mbinu hizo ni ubunifu wa kimuktadha, jozi ya maswali na majibu, vibainishi vya fokasi, usahihishaji wa taarifa, matumizi ya vikumushi vya nomino, muktadha dhahiri, utumiaji wa nahau, muktadha matini na vimaanilizi (picha). Makala hii imejikita katika mbinu ya nahau ili kupima utokeaji wa fokasi katika miundo tofautitofauti ya sentensi za Kiswahili. Uteuzi wa nahau umezingatia kigezo cha maanafiche zinazobebwa na kipera hiki cha fasihi.

Van der Wal (2021) alipendekeza matumizi ya nahau katika kupima mikakati tofautitofauti ya usimbaji wa fokasi katika lugha kadhaa za Kibantu. Miongoni mwa lugha alizoshughulikia ni Kimakua (P31), Kizulu (S42), Kimatengo (N13), Kirundi (JD62), Kichangana (S53), Kiganda (JE15), Kinyakyusa (M31), Kibukusu (JD31c) na Kitharaka (E54). Katika lugha hizo, vijenzi vya nahau viliwekwa katika miundo tofautitofauti ya sentensi ili kupima kama miundo hiyo inatumika kusimba fokasi. Matokeo yalionesha kuwa vijenzi vya nahau vinapowekwa katika miundo tofautitofauti, maana ya nahau inaweza kutoweka au kusalia. Usaliaji wa maana ya nahau hiyo huonesha kuwa muundo huo hautumiki kusimba fokasi katika lugha hiyo. Lakini, maana ya nahau inapotoweka huonesha kuwa muundo husika hutumika kusimba fokasi katika lugha hiyo (van der Wal, 2021). Hata hivyo, tafiti za awali katika lugha ya Kiswahili hazikushughulikia matumizi ya nahau katika ujarabati wa mikakati ya usimbaji wa fokasi. Tafiti hizo zimejikita katika aina, mazingira ya utokeaji wa fokasi na mikakati ya kisarufi inayotumika katika usimbaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili (Taz. Mungania na Schroeder, 2018; Ndumiwe, 2022a; 2022b; 2023). Makala hii ni mwendelezo wa mawazo ya van der Wal (2016, 2021) katika ujarabati wa mikakati tofautitofauti ya usimbaji wa fokasi katika lugha tofautitofauti. Kwa hiyo, mchango wa makala hii ni kuthibitisha madai ya van der Wal (2016, 2021) kuhusu kuwapo kwa mikakati tofautitofati ya usimbaji wa fokasi katika lugha mbalimbali.

Kwa hiyo, lengo kuu la makala hii ni kuchunguza matumizi ya nahau za Kiswahili katika ujarabati wa mikakati ya usimbaji wa fokasi katika sentensi za Kiswahili. Kwa mujibu wa Wamitila (2013), nahau ni kipera cha semi ambacho huwa na kauli fupifupi zinazotumia sana lugha ya picha. Baadhi ya sifa za nahau ni matumizi ya lugha ya mkato, kusitiri maana ya ziada kuliko maana ya msingi ya maneno yanayounda nahau husika, kuundwa na kitenzi na nomino, kuhusisha kauli fupifupi na kuwa na upande mmoja usiohitaji majibu (Skuni, 2018). Huu ni uchunguzi endelevu wa kujarabati mikakati tofautitofauti inayotumika kusimba fokasi katika lugha tofautitofauti.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Uchanganuzi na ufasili wa data za utafiti umeongozwa na Nadharia ya Vibadala vya Kisemantiki iliyoasisiwa na Rooth (2016) ili kushughulikia utokeaji wa fokasi katika lugha tofautitofauti. Nadharia hii inahusu kuwapo kwa vibadala vya fokasi

katika kiambo. Kwa kuzingatia nadharia hii, katika nafasi ya fokasi, kiambajengo kingine chenye hadhi hiyo huweza kutokea. Nadharia hii inafungamana na mtazamo wa Krifka (2007) unaohusu fokasi kama kiashiria cha vibadala vya kimuktadha. Ufasili wa fokasi katika nadharia hii umeegemezwa katika misingi mitatu ambayo ni; kanuni za ung'amuzi wa fokasi, seti ya vibadala vya fokasi katika kiambo na uzalishaji wa vibadala vya kisemantiki katika kiambo. Misingi hii imetumika katika uchanganuzi na ufasili wa data za utafiti huu.

Kuhusu kanuni za ung'amuzi wa fokasi, nadharia hii inaonesha kuwa kuna kanuni tofautitofauti za ung'amuzi wa fokasi katika kiambo. Mojawapo ya kanuni hizo ni ujirani na kitenzi. Kiambajengo chenye hadhi ya fokasi hutokea mara baada ya kitenzi katika lugha zenye muundo wa KTY. Vilevile, kiambajengo hicho hutambuliwa kwa kutumia vibainishi vya fokasi. Vibainishi hivyo hutumika kutambulisha kiambajengo ambacho ni fokasi katika kiambo.

Kwa upande wa seti ya vibadala vya fokasi katika kiambo, nadharia hii inaashiria kuwapo kwa seti za vibadala katika viambajengo vinavyojenga sentensi. Mara nyingi, seti ya vibadala hutegemea muktadha wa kitenzi kilichopo katika sentensi husika. Msingi huu umetumika kung'amua kiambajengo chenye kuchochea seti za vibadala. Kwa kuzingatia utafiti huu, kiambajengo chenye uwezo wa kuchochea seti za vibadala katika muktadha wa kitenzi husika ni nomino inayotokea baada ya kitenzi husika. Kwa hiyo, katika nahau zilizochunguzwa, nomino ya baada ya kitenzi cha nahau ndiyo iliundiwa seti za vibadala vyake ili kupima usimbaji wa fokasi.

Kuhusu uzalishaji wa vibadala vya kisemantiki katika kiambo, Nadharia ya Vibadala vya Kisemantiki inaonesha kuwa uzalishaji wa vibadala ufanyike kwa kuzingatia hadhi ya kiambajengo kinachobadalalishwa. Kwa kuzingatia msingi huu, vijenzi vya nahau vilivyobadalalishwa ni vile vyenye hadhi ya nomino inayotokea baada ya kitenzi. Vijenzi hivi ndivyo vina hadhi ya kuwa fokasi katika sentensi yenye muundo wa Kiima-kitenzi-yambwa au kitenzi-yambwa. Vijenzi hivyo vinapobadalishwa, maana ya nahau inaweza kutoweka au kusalia.

## 3.0 Mbinu za Utafiti

Data za makala hii zilikusanywa kutoka maktabani na uwandani. Kwa upande wa maktabani, nahau 6 zilikusanywa kutoka kwenye andiko la Mauya (2008) na 6 kutoka andiko la Salla (2017) kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka. Maandiko haya yaliteuliwa kwa sababu ndani yake kuna orodha ya nahau zenye maana zake na matumizi ya nahau hizo katika muktadha maalumu. Nahau zilizolengwa ni zile zenye uwezo wa kutumiwa kupima fokasi. Mara nyingi, nahau za namna hiyo huwa na sifa ya kuanza na kitenzi katika muundo wake. Vilevile, nahau zenye uwezo huo hubeba maana tofauti na maana msingi za maneno yanayojenga nahau husika. Kwa mfano, nahau 'vaa miwani' (lewa pombe) na 'changia bia' (fanya jambo kwa ushirika). Nahau hizi zina uwezo wa kuundiwa miundo tofautitofauti ya sentensi kwa sababu zina muundo wa kitenzi na nomino

ndani yake. Baada ya kupata nahau hizo, usampulishaji nasibu sahili ulitumika kupata nahau 12 zilizotumika katika makala hii. Kwa kuzingatia usampulishaji huu, watafiti waliorodhesha nahau 18 zinazoweza kutumiwa kupima fokasi kwenye karatasi; kisha kuzichanganya karatasi hizo na kuziweka mezani. Watafiti waliokota karatasi 12 za kwanza ambapo kila karatasi ilikuwa na nahau yake. Nahau zilizoteuliwa zilitumika kama viwakilishi vya nahau zenye uwezo wa kutumiwa kupima fokasi.

Pamoja na hayo, katika maandiko tajwa, kuna nahau ambazo haziwezi kutumiwa kupima fokasi. Nahau hizo huwa na sifa ya kuanza na nomino katika muundo wake. Vilevile, hutumia maneno yenye maana za kawaida na vijenzi vya nahau hizo. Hii ina maana kwamba maana zake sio za kificho bali zinajulikana. Baadhi ya nahau hizo ni 'ana kwa ana' na 'zungusha mtu'. Aidha, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Toleo la 3 (TUKI, 2013) ilitumika kutoa maana za kawaida za maneno yanayojenga nahau hizo.

Kwa upande wa uwandani, utafiti huu ulifanyika katika Wilaya ya Nyamagana katika Mkoa wa Mwanza. Eneo hilo liliteuliwa kwa sababu ni mojawapo ya maeneo ambayo lugha ya Kiswahili huzungumzwa kutokana na kuwapo kwa makabila tofautitofauti. Aidha, eneo hilo lilitumika kama kiwakilishi cha maeneo mengine yenye wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Katika eneo hilo, watoataarifa 12 wa lugha ya Kiswahili waliteuliwa. Idadi hiyo iliteuliwa ili kila mtoataarifa ashughulikie nahau moja. Watoataarifa hao walikuwa ni walimu wa Kiswahili katika shule nne za sekondari kutoka eneo la utafiti. Shule za sekondari zilizoteuliwa ni Mkolani, Lwanima, Nganza na Buhongwa. Shule hizi ziliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu sahili. Upatikanaji wa watoataarifa hao ulitegemea fursa, yaani aliyekuwapo siku ya kukusanya data ndiye aliyehusika. Aidha, uteuzi wa sampuli hiyo ulizingatia sifa ya elimu ya shahada ya kwanza katika taaluma ya isimu ya lugha ya Kiswahili. Watoataarifa hao walikuwa na jukumu la kutunga sentensi za Kiswahili kwa kutumia vijenzi vya nahau zilizoteuliwa. Kuwapo kwa watoataarifa hao kulitusaidia kupata sentensi tofautitofauti zilizotungwa kwa kuzingatia vijenzi vya nahau. Jambo hili lilitusaidia kung'amua nahau zenye uwezo wa kutumiwa kupima fokasi dhidi ya zile zisizo na uwezo huo. Uchambuzi wa data za utafiti huu umetumia mkabala wa kitaamuli kwa sababu yalihitajika maelezo ya watafiti kuhusu namna nahau zinavyoweza kutumika kung'amua usimbaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umeabainisha kuwa vijenzi vya nahau vinapoundiwa sentensi kwa kutumia mkakati wa ukasimishaji, utenguaji kushoto au upinduzi viambajengo, maana ya nahau hutoweka kabisa. Maana inayotokea baada ya mchakato huo ni ya kawaida ya vijenzi vya sentensi husika. Kwa hiyo, baadhi ya vijenzi vya nahau haviwezi kuchochea seti ya vibadala vingine katika nafasi zake na nahau ikabaki na maana yake (van der Wal, 2021). Kutokana na maelezo hayo, kiambajengo

kisichochochea seti ya vibadala vingine kutokea katika nafasi yake hakiwezi kuwa fokasi (van der Wal, 2021). Kwa mantiki hiyo, seti ya vibadala inapozalishwa, maana ya nahau hutoweka na kubaki maana ya kawaida ya maneno yanayounda nahau hiyo. Mfano wa (3) unatoa mwanga zaidi.

3. (a) Zunguka mbuyu
**Maana ya nahau**: toa rushwa.
**Maana ya kawaida**: enda mwendo wa duara katika mbuyu.
(b) *Zunguka /mwembe/mnazi/mpapai.
**Maana ya nahau:** imepotea
**Maana ya kawaida**: enda mwendo wa duara katika mwembe/mnazi/mpapai.

**Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Mifano ya 3 (a) na (b) inadhihirisha kuwa kutokea kwa vibadala vingine katika mfano 3 (a) husababisha nahau kupoteza maana yake kama ilivyo katika mfano (b). Kwa kuzingatia sfa hii, tunaweza kutumia nahau kupima kama mkakati wa ukasimishaji, utenguaji kushoto au upinduzi viambajengo hutumika kusimba fokasi katika lugha ya Kiswahili. Ubakiaji wa maana ya nahau huonesha kuwa mkakati huo hauwezi kutumika kusimba fokasi katika sentensi. Lakini, maana ya nahau inapotoweka huonesha kuwa mkakati husika hutumika katika usimbaji wa fokasi katika sentensi (van der Wal, 2021).

## 4.1 Ung'amuzi wa Fokasi katika Ukasimishaji

Istilahi '*ukasimishaji*' imetafsiriwa kutoka istilahi ya Kiingereza '*clefting*' yenye maana ya *pasua katika vipande viwili*. Aidha, istilahi '*ukasimishaji*' imetokana na kitenzi "*kasimu*" kilichotoholewa kutoka lugha ya Kiarabu kikiwa na maana ya *kata katikati; fanya sehemu kuwa sawa* (TUKI, 2013: 204). Kwa hiyo, ukasimishaji ni mchakato wa ugawanyaji wa tungo sahili katika vishazi viwili (kishazi huru na tegemezi) kwa lengo la kuonesha taarifa mpya (fokasi) inayokusudiwa kuwasilishwa na mtoataarifa (Lambrecht, 2001a; Dekany, 2010). Mchakato huu ndiyo huunda sentensi kasimio. Sentensi kasimio ni sentensi changamani inayogawanyika katika vishazi viwili ili kuonesha taarifa mpya inayopaswa kumfikia mpokeataarifa (Lambrecht, 2001a na Wakarindi, 2010). Kwa mujibu wa Ndumiwe (2022b), sentensi kasimio katika lugha ya Kiswahili hugawanyika katika aina tatu: sentensi kasimio sahili[4], sentensi kasimio kifani[5] na sentensi kasimio kifani-geuzi[6].

[4] Sentensi kasimio sahili ni tafsiri ya *basic cleft/it-cleft sentence*.
[5] Sentensi kasimio kifani ni tafsiri ya *pseudo-cleft sentence*.
[6] Sentensi kasimio kifani-geuzi ni tafsiri ya *inverted pseudo-cleft sentence*.

Utafiti huu umebaini kuwa nahau huweza kutumiwa kupima fokasi katika sentensi zilizoundwa kwa kutumia mkakati wa ukasimishaji. Baada ya sentensi hizo kuundwa, maana ya nahau huweza kusalia au kutoweka. Usaliaji wa maana ya nahau huonesha kuwa mkakati husika hauwezi kusimba fokasi lakini utowekaji wa maana ya nahau hudhihirisha kuwa mkakati husika hutumika kusimba fokasi katika lugha ya Kiswahili. Maelezo hayo yanawiana na maelezo ya van der Wal (2021) anayeeleza kuwa kiambajengo kisichochochea seti ya vibadala katika nafasi yake hakiwezi kusimbwa kama fokasi. Kutokana na hilo, vijenzi vya nahau vinapokasimiwa ili kuunda sentensi kasimio husababisha maana ya nahau kutoweka na kusalia maana ya kawaida. Kwa hiyo, vijenzi vya nahau haviwezi kuchochea vibadala katika nafasi zake bila kuondosha maana ya nahau husika. Mifano Na. (4) na (5) inadhihirisha ukasimishaji wa vijenzi vya nahau.

**Kabla ya Ukasimishaji**

4. (a) Hasani atachonga mwiko mwezi ujao.
   **Maana ya nahau**: Hasani ataoa mwezi ujao.
   (b) Mvuvi alivuta kamba baada ya jahazi kuzama.
   **Maana ya nahau**: mvuvi alifariki baada ya jahazi kuzama.
   (c) Mwajuma alichungulia kaburi.
   **Maana ya nahau**: Mwajuma alinusurika kufariki dunia.

**Baada ya Ukasimishaji**

5. (a) Ni mwiko utakaochongwa na Hasani mwezi ujao
   **Maana ya nahau**: imepotea
   **Maana ya kawaida:** Hasani atatengeneza mwiko mwezi ujao.
   (b) Kilichovutwa na mvuvi baada ya jahazi kuzama ni kamba
   **Maana ya nahau**: imepotea
   **Maana ya kawaida:** mvuvi aliburuta kamba kwa mikono baada ya jahazi kuzama.
   (c) Kaburi ndilo lililochunguliwa na Mwajuma
   **Maana ya nahau**: imepotea
   **Maana ya kawaida:** Mwajuma alitazama kaburi kupitia upenyo mdogo.

   **Chanzo**: Data za Utafiti (2022)

Kwa kuzingatia Nadharia ya Vibadala vya Kisemantiki, viambajengo ‘mwiko’, ‘kamba’ na ‘kaburi’ katika Mfano Na. 4 (a)-(c) ndivyo vyenye uwezo wa kuchochea vibadala katika nafasi zake kwa sababu vinatokea baada ya kitenzi kikuu. Aidha, viambajengo baada ya kuundiwa sentensi kasimio ndivyo vimetambulishwa kwa kutumia vibainishi vya fokasi ‘ni’ na ‘ndilo’ katika mfano wa 5(a)-(c). Vibainishi hivi hutumika kutambulisha fokasi inayotokea kabla au baada ya kibainishi hicho (Ndumiwe, 2023).

Kupitia Mfano Na. 5 (a)-(c), inabainika kuwa maana ya nahau imetoweka baada ya ukasimishaji wa vijenzi vya nahau ilhali katika Mfano Na. 4 (a)-(c) kabla ya ukasimishaji, nahau zina maana zake. Aidha, aina zote tatu za sentensi

kasimiwa zimejitokeza katika Mfano Na. 5 (a)-(c) ambapo (a) ni kasimio sahili, (b) ni kasimio kifani na (c) ni kasimio kifani-geuzi. Kwa hiyo, udondoshi wa maana ya nahau baada ya ukasimishaji unaonesha kuwa mkakati husika unatumika katika usimbaji wa fokasi katika lugha ya Kiswahili.

**4.2 Ung'amuzi wa Fokasi katika Upinduzi wa Viambajengo**

Upinduzi wa viambajengo ni mabadiliko ya mpangilio wa kawaida wa vijenzi vya sentensi (Marten na van der Wal, 2014). Katika mabadiliko haya, vijenzi vya sentensi msingi huhamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kutegemeana na dhamira ya msemaji au mwandishi wa tungo husika. Upinduzi wa viambajengo katika lugha nyingi za Kibantu huhusisha kirai nomino (KN) kinachotokea kabla ya kitenzi na kirai nomino (KN) kinachotokea baada ya kitenzi (Marten na Gibson, 2015). Tafiti za awali zinaonesha kuwapo kwa aina nne za upinduzi wa viambajengo katika lugha za Kibantu. Aina hizo ni upinduzi wa kimahali, kiathirika, ala (kitumizi) na wa kijalizo (Zeller, 2012; Marten na Gibson, 2015; Hassan, 2019). Vilevile, tungo zenye upinduzi wa viambajengo katika lugha za Kibantu zina sifa zifuatazo: (1) kiima hudhibiti upatanisho wa kisarufi, (2) upatanishi wa yambwa hautokei katika tungo zenye upinduzi wa viambajengo, (3) ubadilikaji wa dhima za kisemantiki za vijenzi vya tungo na (4) KN kabla ya kitenzi ni mada ilhali KN baada ya kitenzi ni fokasi.

Katika utafiti huu imebainika kuwa vijenzi vya nahau vinapopinduliwa maana ya nahau hutoweka au kusalia. Usaliaji wa maana ya nahau hudhihirisha kuwa mkakati husika hauwezi kusimba fokasi katika lugha ilhali utowekaji wa maana ya nahau hudhihirisha kuwa mkakati husika husimba fokasi katika lugha ya Kiswahili. Mifano Na.a (6) na (7) inadhihirisha haya.

**Kabla ya Upinduzi wa Viambajengo**

6. (a) Mama amevunja nyumba ya mtoto.
**Maana ya nahau**: mama ameharibu ndoa ya mtoto.
(b) Wafugaji walizunguka mbuyu.
**Maana ya nahau**: wafugaji walitoa rushwa
(c) Ashura alivunja zizi wakati wa harusi yake.
**Maana ya nahau**: Ashura alikiuka maadili wakati wa kufunga ndoa.

**Baada ya Upinduzi wa Viambajengo**

7. (a) Nyumba ya mtoto ilivunjwa na mama.
**Maana ya nahau**: imepotea
**Maana ya kawaida:** jengo la kuishi la mtoto liliharibiwa na mama yake.
(b) Mbuyu ulizungukwa na wafugaji.
**Maana ya nahau**: imepotea
**Maana ya kawaida:** mti uitwao mbuyu ulizungukwa na wafugaji.
(c) Zizi lilivunjwa na Ashura wakati wa harusi yake.
**Maana ya nahau**: imepotea
**Maana ya kawaida:** zizi liliharibiwa na Ashura wakati wa harusi yake.

**Chanzo**: Data za Utafiti (2022)

Viambajengo katika Mfano Na. 6 (a)-(c) vinaonesha nahau katika tungo za Kiswahili zikiwa na maana yake ilhali katika Mfano Na.7 (a)-(c) baada ya upinduzi wa viambajengo maana ya nahau imetoweka. Utowekaji wa maana ya nahau unathibitisha kuwa mkakati wa upinduzi wa viambajengo hutumika kusimba fokasi katika lugha ya Kiswahili. Aidha, mifano katika Na. 7 (a)-(c) ni upinduzi wa kiathirika.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Vibadala vya Kisemantiki, viambajengo 'nyumba ya mtoto', 'mbuyu' na 'zizi' katika Mfano Na. 6 (a)-(c) ndivyo vyenye uwezo wa kuchochea vibadala katika nafasi zake kwa sababu vinatokea baada ya kitenzi kikuu. Aidha, baada ya viambajengo hivyo kupinduliwa, vimepoteza sifa ya kuwa fokasi kwa sababu vimetokea kabla ya kitenzi. Kwa hiyo, viambajengo 'mama', 'wafugaji' na 'Ashura' katika Mfano Na. 7 (a)-(c) ndivyo vimekuwa fokasi kwa sababu vimetokea jirani na kitenzi. Kwa hiyo, upinduzi wa viambajengo ni mkakati mmojawapo unaotumika kusimba fokasi katika lugha ya Kiswahili.

**4.3 Ung'amuzi wa Fokasi katika Mkakati wa Utenguaji Kushoto**

Utenguaji kushoto[7] ni mkakati wa uondoaji wa kishiriki cha kitenzi (yambwa) katika nafasi yake ya asili katika muundo msingi na kukihamishia katika ukingo wa kushoto wa sentensi (Lambrecht, 2001b). Aidha, Zeller (2004) anasisitiza kuwa tungo za utenguaji kushoto hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine kutokana na tofauti za miundo msingi ya lugha husika. Tungo zenye utenguzi wa kushoto katika lugha ya Kiswahili huwa na sifa zifuatazo: mosi, kiambajengo tenguliwa hutenganishwa kwa pumziko fupi na sehemu zingine za sentensi. Katika uandishi, sifa hiyo hudhihirishwa kwa alama ya mkato inayowekwa kati ya kiambajengo tenguliwa na sehemu zingine za sentensi. Pili, kiambajengo tenguliwa sharti kipatanishwe na kiambishi cha yambwa kinachopachikwa katika kitenzi. Tatu, kiambajengo tenguliwa hakiongozi upatanisho wa kisarufi wa kiima-kitenzi bali sentensi hubakia na upatanisho kama ilivyokuwa kabla ya utenguaji, yaani, kiima huendelea kuongoza upatanisho wa kisarufi kati ya kiima na kitenzi. Nne, muundo msingi wa lugha hubadilika kutoka kiima-kitenzi-yambwa (KTY) kuwa yambwa-kiima-kitenzi (YKT). Hii ni kutokana na yambwa inayobeba 'fokasi' kutenguliwa na kuwekwa kushoto mwa sentensi. Sifa hizo zinadhihirika katika Mfano Na. 8 na 9.

8. (a) Kijiji kimekumbatia rufani
kng7-jiji kp7-tmlf-kumbati-kt Ørufani
'Kijiji kimekumbatia rufani'.

(b) Babu aliangukia mtungi mwaka jana.

[7] Utenguaji kushoto ni tafsiri ya *left dislocation* kutoka lugha ya Kiingereza.

babu knf-knj-anguki-kt kng3-tungi kng3-aka jana
'babu aliuangukia mtungi mwaka jana'.

9. (a) **[Rufani]F**, ki-jiji ki-me-i-kumbati-a.
Ørufani kng7-jiji kp7-tmlf-ky-kumbati-kt
'Rufani, kijiji kimeikumbatia'

(b) **[M-tungi]F,** babu a-li-u-anguki-a mw-aka jana
kng3-tungi babu knf-knj-ky-anguki-kt kng3-aka jana
'mtungi, babu aliuangukia mwaka jana'.

**Chanzo**: Data za Utafiti (2022)

Tungo katika Mfano Na. 8 (a) na (b) zina mpangilio sahili wa viambajengo vyake kabla ya utenguaji kushoto. Maneno 'rufani' na 'mtungi' katika Mfano Na. 9 (a) na (b) ni fokasi zilizosimbwa na mkakati wa utenguaji kushoto. Fokasi hizi zimetenganishwa kwa pumziko fupi katika sentensi hizo. Pia, zinapatanishwa na kiambishi yambwa {-i-} na {-u-} katika kitenzi *kimeikumbatia* na *aliuangukia*. Vilevile, viima *kijiji* na *babu* ndivyo vimeongoza upatanisho wa kisarufi wa kiima-kitenzi. Kadhalika, muundo msingi wa lugha umekuwa yambwa-kiima-kitenzi katika sentensi zilizotenguliwa.

Katika utafiti huu, imebainika kuwa yambwa inapotenguliwa kuelekea kushoto katika tungo iliyoundwa kwa kutumia nahau maana ya nahau inaweza kutoweka au kusalia. Ubakiaji wa maana ya nahau huonesha kuwa mkakati wa utenguaji kushoto hauwezi kusimba fokasi lakini utowekaji wa maana ya nahau hudhihirisha kuwa mkakati madhukura hutumika kusimba fokasi. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya.

### Kabla ya Utenguaji Kushoto

10. (a) Juma alimwaga unga katikati ya umati wa watu.
**Maana ya nahau**: Juma alipoteza ajira katikati ya umati wa watu.
(b) Fundi nguo alikanyaga nyaya ofisini kwake.
**Maana ya nahau**: Fundi nguo alipata maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi akiwa kazini kwake.
(c) Mwajuma alivunja ungo akiwa jikoni.
**Maana ya nahau**: Mwajuma alipata hedhi ya kwanza akiwa jikoni.

### Baada ya Utenguaji Kushoto

11. (a) Unga, Juma ali-u-mwaga katikati ya umati wa watu.
**Maana ya nahau**: imepotea
**Maana ya kawaida:** Juma alisambaza unga katikati ya watu.
(b) Nyaya, fundinguo alizikanyaga ofisini kwake.
**Maana ya nahau**: imepotea

**Maana ya kawaida:** Fundinguo aligandamiza nyaya kwa nyayo akiwa eneo lake la kazi.

(c) Ungo, Mwajuma aliuvunja akiwa jikoni.

**Maana ya nahau**: imepotea

**Maana ya kawaida:** Mwajuma alipasua ungo katika vipandevipande akiwa jikoni.

**Chanzo**: Data za Utafiti (2022)

Katika Mfano Na. 10(a)-(c), kuna mpangilio wa kawaida wa vijenzi vya sentensi, yaani kabla ya utenguaji kushoto. Katika mpangilio huo, nahau zimewekwa kwenye tungo na huendelea kuhodhi maana ya nahau. Hata hivyo, baada ya utenguaji kushoto, katika Mfano Na. 11 (a)-(c), maana za nahau zimetoweka na kusababisha tungo iliyoundwa kuwa na maana ya kawaida. Kutokana na hilo, tunang'amua kuwa mkakati huu hutumika kusimba fokasi katika lugha ya Kiswahili. Maelezo haya yanafungamana na maelezo ya van der Wal (2021) anayoeleza kuwa maana ya nahau inapotoweka huonesha kuwa mkakati husika hutumika katika usimbaji wa fokasi.

Kwa kurejelea Nadharia ya Vibadala vya Kisemantiki, viambajengo 'unga', 'nyaya' na 'ungo' katika Mfano Na. 15 (a)-(c), ndivyo vyenye uwezo wa kuchochea vibadala katika nafasi zake kwa sababu vinatokea baada ya kitenzi kikuu. Aidha, baada ya viambajengo hivyo kutenguliwa kushoto, vimeendelea kufungamana na kitenzi kwa kutumia kiambishi yambwa kinachotokea ndani ya vitenzi husika. Viambajengo hivyo vimebeba fokasi kwa sababu vimebeba taaarifa mpya katika kiambo. Kwa hiyo, utenguaji kushoto ni mkakati mmojawapo unaotumika kusimba fokasi katika lugha ya Kiswahili.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii ilikusudia kuthibitisha madai ya van der Wal (2021) kwa kutumia nahau za lugha ya Kiswahili. Van der Wal (2021) alidai kuwa nahau zinaweza kutumika kupima mikakati ya usimbaji fokasi katika lugha za Kibantu. Nahau zilizotumika zimewekwa katika mikakati mitatu ya usimbaji wa fokasi: ukasimishaji, upinduzi wa viambajengo na utenguaji kushoto. Kwa hiyo, utafiti huu umebaini ung'amuzi wa fokasi katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia nahau. Kwa kawaida, kiambajengo ambacho ni fokasi sharti kichochee kutokea kwa vibadala vingine katika nafasi zake. Hata hivyo, vijenzi vya nahau haviwezi kuchochea vibadala vingine bila kathiri maana ya nahau. Kwa hiyo, vijenzi vya nahau vinapopitia katika mikakati ya kisintaksia maana ya nahau inatoweka au kusalia maana ya kawaida ya vijenzi vya tungo. Kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa utowekaji wa maana ya nahau huonesha kuwa mkakati husika hutumika kung'amua usimbaji wa fokasi katika lugha za Kibantu, kinyume chake maana ya nahau inaposalia huonesha kuwa mkakati husika hautumiki kusimba fokasi katika lugha ya Kiswahili. Aidha, tunapendekeza maeneo mengine ambayo tafiti zingine za namna hii zinaweza kufanyika. Mathalani, ung'amuzi wa fokasi

katika vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile hadithi, methali, mafumbo, vitendewili na sitiari.

**Marejeleo**

Dekany, E. (2010). "The English Cleft Construction It-clefts". *The Odd Yearbook*. 8: 39-78.

Gundell, J., Nancy, H. na Ron, Z. (1993). "Cognitive Status and the Reform of Referring Expression in Discourse". *Language*. 69(2): 274-307.

Hassan, F. (2019). *Uchanganuzi wa Upinduzi wa Kimahali katika Lugha ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Krifka, M. (2007). "Basic Notions of Information Structure." *Interdisciplinary Studies on Structure*. 6: 13-55.

Kroeger, P.R. (2012). "Serial Verb Construction in Balinese: Syntactic and Semantic Analysis". *e-Journal of Linguistic*. 6 (1): 24-42.

Lafkioui, M.B., Nshemezimana, E. na Bostoen, K. (2016). "Cleft Constructions and Focus in Kirundi". *Africana Linguistica*. 22:71-106.

Lambrecht, K. (2001a). "A Framework for Analysis of Cleft Constructions." *Linguistics*. 39 (1): 463-516.

Lambrecht, K. (2001b). "Dislocation." Katika M. Haspelmath, E. Konig, W. Oesterreicher, na W. Raible (Wah.), *Typology and Language Universals.* Berlin: Walter de Gruyter. Kur. 1050-1078.

Marten, L. na Gibson, H. (2015). "Structure Bulding and Thematic Constraints in Bantu Inversion Constructions". *Journal of Linguistics*. 52(3): 565-607.

Marten, L. na van der Wal, J. (2014). "A typology of Bantu Subject Inversion." *Linguistic Variation.* 14 (2): 317-368.

Mauya, A.B. (2008). *Semi: Maana na Matumizi* (Chapa ya Pili). Dar es Salaam: TUKI

Morimoto, Y. (2014). *Focus Marking in Kikuyu (E51)*. Kongamano la Kimataifa la 8 la Lugha za Kibantu. Lilifanyika tarehe 1 Machi 2014, London.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu.* Dar es Salaam: KAUTTU.

Mungania, B.G. na Schroeder, H. (2018). "Topic, Focus and Word Order in Kiswahili Clause". *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics*. 7: 114-138.

Mwamzandi, M.Y. (2014). *Swahili Word Oder Choices: Insight from Information Structure*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Texas.

Ndumiwe, E.J. (2022a). "Fokasi: Misingi ya Uainishaji, Mbinu za Ung'amuzi na Mikakati ya Usimbaji katika Sentensi za Kiswahili". *Nuru ya Kiswahili*. 1(2): 106-134.

Ndumiwe, E.J. (2022b). “Unyambuaji wa Kitenzi na Athari zake katika Usimbaji wa Mada na Fokasi katika Sentensi za Kiswahili”. *Journal of Linguistics and Language in Education*. 16(2): 20-38.

Ndumiwe, E.J. (2023). *Uchunguzi wa Usimbaji wa Fokasi Katika Sentensi za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ngonyani, D. (1998). “Properties of Applied Objects in Kiswahili and Kindendeule”. *Studies in African Linguistics*. 27(1): 67-95.

Rooth, M. (2016). “Alternative Semantics”. Katika C. Féry na S. Ishihara (Wah.), *The Oxford Handbook of Information Structure*. Oxford: Oxford University Press. Kur. 260 - 288.

Salla, H.D. (2017). *Nahau za Kwetu 1*. Dar es Salaam: APE Network.

Skuni, M.M. (2018). *Kuchunguza Jinsi Nahau za Kiswahili Sanifu Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lugha*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: Oxford University Press.

van der Wal, J. (2009). *Word Oder and Information Structure in Makhuwa-Enahara*. Leiden: LOT.

Van der Wal, J. (2016). “Diagnosing Focus”. *Studies in Language.* 40(2): 259-301.

Van der Wal, J. (2021). “On the Use of Idioms for Testing Focus”. *Semantic Field Method*. 3 (3):1-17.

Wakarindi, P.M. (2010). *A Functional Grammar Approach to the Analysis of Gikuyu Emphatic Clauses*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wamitila, K.W. (2013). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Yonenda, N. (2011). “Word Order in Matengo (N31): Topicality and Information Roles”. *Lingua*. 121: 754-771.

Zeller, J. (2004). “Left Dislocation in Zulu.” *Southern African Linguistics and Applied Language Studies*. 22(1-2): 75-93.

Zeller, J. (2012). “Instrument Inversion in Zulu”. Katika R. Michael, B.N. Marlo, R.C. Adams, M.M. Green, na P.M Tristan (Wah.), *42nd Annual Conference on African Linguistics*. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. Kur. 134-148.